

MIFUPA 206

Gabbi Masebo ametoweka kusikojulikana wala kaburi lake halifahamiki lilipo. Harakati za kumtafuta zilizofanyika kwa muongo mmoja zinagonga mwamba na faili lake linafungwa na kutupwa kando - *Closed and abandoned*

"Bado sijaridhika" Chaz Siga mpelelezi mahiri anajiambia huku akijiuliza "Yawezekana vipi kwa mwanausalama huyu makini atoweke muda mfupi tu baada ya kufunga ndoa na msichana mrembo ambaye kwa kipindi kirefu amekuwa habari ya jiji la Dar es Salaam?"

Turufu yake inaangukia Vampire Casino, kisima cha starehe chenye ladha tofauti za wanawake na bidhaa zote za shetani ili kukutana na Milla Cash, msichana mlimbwende na kahaba *professional*

Kuonekana tena kwa marehemu Tiglis Tsega, askari koplo, komandoo na mdunguaji hatari wa jeshi akirandaranda mitaani kunaamsha hisia mpya na Mifupa 206 inagundulika chini ya daraja la Surrender - Dar es Salaam. Chaz Siga anapiga chafya kali... "Huu ni mchezo mchafu"



"Riwaya tamu zaidi ya kijasusi na mapenzi kuwahi kuandikwa nchini Tanzania" - Jueni S. Musimu

"Mifupa 206 ni zaidi ya Riwaya zote nilizowahi kusoma" - Erick D. Sanga



Kevin e. Mponda

MIFUPA 206

MIFUPA 206

Kipimo kwa kipimo RIWAYA



KEVIN E. MPONDA

MWANDISHI WA RIWAYA TAI KWENYE MZOGA